

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA
(Barua zote zielekezwe Kwa Mkurugenzi wa Halmashauri)

☎ Simu: Na : 026 -2702647

📠 Faksi Na : 026 - 2702203



Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa,
S.L.P 162,
IRINGA.

Kumb. Na. IMC/S.20/2/VOL.I/117

Tarehe 23/02/2021

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa amepokea kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb Na. FA.170/363/01"A"41 cha tarehe 10 Februari, 2021. Ili kuziba nafasi hizo Mkurugenzi anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na umri wa miaka 18 hadi 45 kuomba nafasi hizo.

1) KATIBU MAHSUSI III – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 1)

Majukumu ya kazi

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasilisha shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka na kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kuwaarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

Sifa za Waombaji

Waombaji wawe wamehitimu kidato cha nne au cha sita, waliohudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya 'Kompyuta' kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

2) MTENDAJI WA MTAI III – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 1)

MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTAI III

- i. Katibu wa Kamati ya Mtaa.
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa.
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- iv. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa.
- v. Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- vi. Mshauri wa kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama.
- vii. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ix. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa.
- x. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

Sifa za Waombaji

Waombaji wawe wamehitimu kidato cha nne (IV) au sita (VI). Waliohitimu mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.


MASHARTI KWA UJUMLA

- i. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi katika Idara yoyote atakayopangiwa.
- ii. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- iii. Mwombaji aambatishe maelezo yake binafsi (CV).

- iv. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vya Taaluma, vyeti vya Kidato cha IV, Cheti cha Kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma, nakala hizo zithibitishwe na Hakimu au Wakili.
- v. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe tarehe **10 March, 2021 Saa 9:30 Alasiri.**

Maombi hayo yatumwe kwa anwani ifuatayo;-

MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA,
S.L.P. 162,
IRINGA.



HAMID A. NJOVU
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA IRINGA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
IRINGA**